# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI

**Mawasiliano:**

**Mkuu wa shule**: **0764099034**

**Makamu mkuu wa shule**: **0620122644**

**Email**: bugandosecondary@gmail.com

**Shule ya sekondari Bugando,**

**S.L.P 151,**

**GEITA.**

**Tarehe………………**

**Kumb.Na BSS/F5/2024/1**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…………………**

**……………………………………………………...**

**S.L.P…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUGANDO HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA KIDATO CHA TANO MWAKA …………..**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule h**ii** mwaka **………..** tahasusi ya…………………,shule ya sekondari Bugando ipo umbali wa kilometa 44 kaskazini magharibi kutoka mjini Geita. Kufika shuleni panda basi au gari zinazoelekea NZERA makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya GEITA , ukifika NZERA panda bodaboda hadi shuleni (nauli ya bodaboda ni shilingi 2000/ =). Muhula wa masomo unaanza tarehe **………...** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni ***Tarehe ……….***. Na mwisho wa kuripoti ni **Tarehe ………….**

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**:

1. **SARE ZA SHULE**.
   - (a) Sare ya shule h**ii** ni mashati mawili (2) meupe ya tetron yenye mikono mirefu.
   - (b) Suruali mbili(2) rangi ya **kijivu giza** zenye malinda manne (4) (malinda mawili upande wa kulia na mawili upande wa kushoto.
   - (c) Sare ya michezo ni trucksuit na kaptula mbili (02) za rangi ya **bluu** ivuke magoti **siyo suruali** ikiwa na vest yake vinauzwa pamoja.Hakikisha unakujanavyo, **Kumbuka** pia kuja na raba jozi moja (1) kwa ajili ya michezo.
   - (d) Viatu vya shule ni **vyeus**i vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi mbili.
   - (e) Soksi fupi jozi mbili (2) rangi **nyeusi**.
   - (f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.

(g) Sweta rangi ya **dark bluu** inapatikana madukani.
(h) Tai mbili (2) rangi ya kijivu giza.
(i) -Nguo za kushindia ni tisheti ya shule rangi ya **dark blue** yenye kola ya rangi ya **kaki**
-Suruali ya kushindia rangi **nyeusi** yenye malinda mawili kila upande.

**KUMBUKA**:Shati la shule litachomekewa muda wote unapovaa sare ya shule.

2. **UVAAJI WA SARE YA SHULE.**

Sare ya shule inavaliwa wakati wote wa masomo,baraza,mihadhara na wakati Mwanafunzi anapokwenda nje ya mipaka ya shule kama vile kanisani, msikitini n.k. T.shirt ya shule ivaliwe shuleni tu wakati usio wa masomo na sweta livaliwe wakati wa Baridi tu. Majaketi,kofia,makoti,na mapambo mengine haviruhuisiwi kuvaliwa kabisa pamoja na sare ya shule.Hivyo atakayeonekana na mavazi tofauti na yaliyoainishwa Hapo juu atachukuliwa hatua za kinidhamu.

**KUMBUKA**: NGUO ZINGINE ZOZOTE TOFAUTI NA SARE YA SHULE HAZIRUHUSIWI KUVALIWA SHULENI NA NJE YA SHULE NA IKITOKEA UMEZIVAA ZITAKAMATWA NA HAZITARUDISHWA NA HATUA KALI ZA KINIDHAMU ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO.

3. **MICHANGO YA SHULE**.

Mwanafunzi wa bweni atalipa Michango kwenye akaunti ya shule,
**SHULE YA SEKONDARI BUGANDO AKAUNTI NAMBA 31001100550 KATIKA BENKI YA NMB.**
Unatakiwa ukabidhi stakabadhi kabla Hujasajiliwa (tafadhali andika jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi yake nyuma ya stakabadhi au pay in slip).

(a) KWA WANAFUNZI WA BWENI

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **Jumla** | | **80,000/=** |

- **MUHIMU**: Mwanafunzi aje na Bima ya Afya au kama hana aje na Pesa kwa ajili ya bima Tshs. 50,400/= (*Fedha taslimu*).

4. **MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI**:

(a) Ream mbili za karatasi (2) aina ya A4 (kwa mwaka).
(b) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
(c) Scientific calculator silent non programmable with function ranging from FX-82 to Fx-991 kwa wale wanaosoma tahasusi za HGL, PCB na PCM na mathematical set.
(d) Dissecting kit kwa wale wanaosoma tahasusi ya PCB
(e) Godoro kwa wanafunzi wa bweni futi 6 kwa futi 2.5
(f) Shuka jozi mbili (rangi ya pink), blanketi-1,foronya-1,chandarua-1(**shuka la kimasai hairuhusiwi na halitambuliki kama shuka au blanketi).**
(g) Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe)
(h) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
(i) Jembe na mpini **(kwa wanafunzi wa PCB na PCM tu**)
(j) Kwanja-1,reki-1, mfagio wa ndani (soft bloom)-1 na Mfagio wa nje (chelewa)-1 na mopper-1.
(k) Mfagio mgumu wa usafi/Hard broom-1 na brashi ya choo/Toilet brush-1 (**kwa wanafunzi wa HGL tu**).
(l) Jalada (file cover) la kutunzia kumbukumbu zako.
(m) Vifaa vya usafi (mswaki, dawa ya meno,dawa ya viatu, kioo,Kitana ,kanda mbili, taulo nk)
(n) Madaftari (counter books) yasiyo pungua saba (7), madaftari ya kawaida na Grafu kwa ajili ya mazoezi.
(o) Sanduku imara na kufuli madhubuti kwa ajili ya kutunzia mali zako.
(p) Dumu la lita 5 la kutunzia maji ya kunywa.

5. **KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE YA SEKONDARI BUGANDO:**
**MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**:

(i)Wizi.
(ii)Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku tisini bila taarifa/utoro.
(iii)Kugoma, kukataa adhabu halali au kuhamasisha mgomo.
(iv)Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu,walezi na jamii kwa ujumla.
(v)Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule.
(vi)Kufuga ndevu au kufuga nywele.
(vii)Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(viii)Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya au biashara yoyote ya madawa ya kulevya.
(ix)Uvutaji wa sigara.
(x)Uasherati, mahusiano ya jinsia moja au kuoa.
(xi)Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xii)Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xiii)Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xiv)Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi (kifaa cha mawasiliano) katika mazingira ya shule kinyume na utaratibu.
(xv)Kudharau bendera ya Taifa.

(xvi)Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.
(xvii)Uharibifu wamali za umma kwa makusudi.

6. **VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**.

- Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki Katika mgomo,fujo na makosa yajinai.
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa michango na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
- Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu na mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
- Sheria na kanuni za shule ya sekondari ya Bugando.
- Kivuli cha matokeo ya mtihani wa kidato cha nne 2022
- Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi au walezi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO, WASILIANA NA SHULE ILI KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO;**

**Mkuu wa shule: 0764099034.**

**Makamu mkuu wa shule: 0620122644.**

**Mwandamizi taaluma: 0623212118**

**Mwandamizi mlezi: 0765180521**

7. **Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBUNI SANA**




**Peter M. Mayala**
**MKUU WA SHULE**

***KIAMBATANISHO A***

**A. ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI (COMBINATION)**

VITABU VINAVYOTUMIKA NI VYA MTAALA MPYA.

**PCM:**

1. **PHYSICS**
2. **CHEMISTRY**
3. **ADVANCED MATHEMATICS**

**PCB:**

1. **PHYSICS**
2. **CHEMISTRY**
3. **BIOLOGY**
4. **BASIC APPLIED MATHEMATICS**

**HGL**

1. **HISTORY**
2. **GEOGRAPHY**
3. **ENGLISH LANGUAGE**

**NB: Masomo ya lazima kwa tahasusi zote ni:**

1. **Academic communication.**
2. **Historia ya Tanzania na maadili.**

1. PHYSICS REFERENCE BOOKS
   Mehta.v.k, (2013) S. Chand's principles of Physics for Class xll 7th ED,S. Chand & Company pvt Ltd, New
2. CHEMISTRY REFERENCE BOOKS 1. Jain.S.K,(2010),Conceptual chemistry For Classx1,S.Chand & Company Ltd New Delhi, india. 2. Bahl. B.S et al (2009), Essentials of physical chemistry, s, chand & company Ltd, New Delhi, india. 3. Ramsden. E.N, (2000), A-Level chemistry, 4th Ed, Nelson Thorns Ltd, U.K.
3. BIOLOGY REFERENCE BOOKS.
   Taylor D.J,(1999),Biological Science,3rd Ed,Cambridge University Press London Understanding Biology
4. ADVANCED MATHEMATICS REFERENCE BOOKS. 1. Horril.P.J.F.(1985),Pure Mathematics Book 2,3rd Ed, Longman Group Limited, London. 2. Tranter. C.J. (1975), Advanced level pure mathematics, 4th Ed, Hodder & Stoughton, London. 3. Dass. H. K & Verma, R. (1997) S.chand'smathematics for class xii (volume ii), S.chand & Compan ltd. New delhi.
5. ENGLISH LANGUAGE REFERENCE BOOKS 1. Francis Mnyawi, Contemporary English. 2. Nicolous Ashel (2016), Advanced English Language 3. Ndambo, English Language for Advanced Level; Nyambari Nyangwine.
6. GEOGRAPHY REFERENCE BOOKS
   1. Bunnett R.B (2006), General Geography in Diagrams, Pearson Education South Asia, Ptc Ltd Singapore.
   2. Monk House F.J(1975), Principles of Physical Geography.
   3. Leong C.G and Morgan C.G (2009), Human and Economic Geography, Oxford University Press. UK
   4. Avelius Thobias (2001), Fundamental in Advanced Level Practical Geography, Mwagomba Press, Dar es Salaam. (kinapatikana shuleni kwa Tshs.16,000/=)

7. HISTORY REFERENCE BOOKS
   1. Avelius Thobias (2001), Fundamental in Advanced Level History 1, Mwagomba Press, Dar es Salaam. (kinapatikana shuleni kwa Tshs.16,000/=)
   2. Avelius Thobias (2001), Fundamental in Advanced Level History 2, Mwagomba Press, Dar es Salaam. (kinapatikana shuleni kwa Tshs.16,000/=)

**B. TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina la Mwanafunzi……………………………………………………………………………….…
2. Tarehe ya Kuzaliwa…………………….Mwezi:……………………Mwaka……………………………..
3.Amezaliwa katika Wilaya ya ………………………………………………………………………..……
4. Uraia……………………………………………………………………………………………..…
5. Shule anakotoka……………………………………………………………………………………..….
6.Mahali anapoishi kwa sasa …………………Wilaya ya ……………tarafa……………………………..…..
Kata…………………………………………………….Mtaa……………………..……………………..….
7. Dini………………………………………………………………………………...……………..…
8. Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………(a)Kazi………..…………………..……………
(b)Anwani ya Mzazi/Mlezi…………………………………………Mabadiliko ya wasilishwe ofisini maramoja (c)Simu ya Nyumbani/Mkononi……………………………(Nimuhimu kwa mawasiliano ya dharura)
9. Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali wala siyo ya DINI Fulani. Aidha inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu. Hivyo, kila siku ya Ijumaa, Jumamosi na Jumapili wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao. Aidha,kumepangwa vipindi viwili vya dini katika ratiba ya masomo kwa siku ya jumatano na kila siku jioni baada ya chakula kuanzia Saa1.00–1.30 usiku. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule. Mzazi amshauri mtoto vizuri kuzingatia agizo hili bila kuleta sababu zozote.
10.**Ahadi ya Mwanafunzi**: Mimi……………………………Ninakubali/Sikubali nafasi niliyopewa Naahidi/Siahidi kutii kikamilifu kanuni,Sheria na maagizo ya shule na ndiyo mwongozo wangu mpaka kumaliza Shule. Sahihi ya Mwanafunzi:………………………………..………………………
11.Mimi Mzazi/Mlezi………………………………Nakubaliana/Sikubaliani na maagizo yaliyotolewa hapo juu.

Jina la Mzazi/Mlezi:……………………………Tarehe:……………………………

**NB**.Mzazi/Ndg.ambaye picha yake haipo katika fomu hii haruhusiwi kuja kumwona mwanafunzi.

**PICHA NAMBA 1** **PICHA NAMBA 2** **PICHA NAMBA 3** **PICHA NAMBA 4**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |

**C: RANGI ZA SARE ZA SHULE ZA WANAFUNZI**

1.RANGI YA SURUALI NI KIJIVU GIZA (KITAMBAA AINA YA CRETA)



2.T-SHIRT NI DARK BLUU YENYE KOLA YA KAKI



3.RANGI YA SWETA NI DARK BLUU



4.RANGI YA TRACKSUIT NI BLUU



**D. STUDENTS MEDICAL CERTIFICATE.**

To be completed by the Government Medical Office and return to the Headmaster, Bugando Secondary school, put tick to the respective response, **Name**: …………………………………………

Please examine the student named above and comment on his health by responding to the following items.

Kindly put a tick (√) in front of either YES or NO whichever is applicable.

A: Sight? 1. NO 2YES: If YES State…………………………………………………

B: Hearing? 1.NO 2YES: If YES State………………………………………………….

C: T.B?. 1NO 2 YES If YES State………………………………………………

D:Blood Pressure 1NO 2YES If YES State…………………………………………

E: A STHMA 1NO 2YES If YES State…………………………………………………..

F: Any other health problems 1NO 2YES If YES State…………………………………

G: Any physical Disability? 1NO 2 YES If YES State…………………………………

Do you therefore recommend the said student medically fit for student at this school?1.NO 2.YES

If No please state: ………………………………………………………………….

Name and signature: ……………………………………………………………..

Designation……….………………………Date……..……………………………...

Official Stamp…………...............................